**MULIKA Na. 39 2020 (66-78)**

# Njia za Usawirishwaji wa Sihiri kwenye Utendi wa *Rukiza* na Dhima zake katika Kumpambanua Shujaa wa Kiutendi

Christopher B. Lucas na Ramadhani T. Kadallah[1]

Chuo Kikuu cha Mt. Augustino na Chuo Kikuu cha D ar es Salaam

**Ikisiri**

Makala haya yamejihusisha na jinsi sihiri ilivyosawiriwa katika utendi wa *Rukiza*. Aidha, uchunguzi huu umechochewa na kuwapo kwa mgongano wa hoja baina ya wataalamu kuhusu matumizi ya sihiri katika kumjenga shujaa na kupambanua vipengele vingine vya kiutendi katika fasihi ya Kiafrika. Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa njia ya maktaba na ilichambuliwa kwa kuzingatia mkabala wa kitaamuli. Kadhalika, Nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe ndiyo iliyotumika kama dira ya kufikia matokeo ya utafiti huu. Matokeo yaliyopatikana baada ya uchambuzi wa data yanaonyesha kwamba sihiri husawiriwa kwa kutumia njia mbalimbali kama vile miujiza, sadaka, ramli, siri, nguvu za ajabu na ndumba. Kutokana na matokeo hayo, imehitimishwa kwamba sihiri ni kipengele muhimu sana katika fasihi ya Kiafrika, hasa katika tendi kwa kuwa pamoja na mambo mengine husaidia kupambanua nduni mbalimbali walizonazo mashujaa. Kushamiri kwa matumizi ya sihiri katika tendi kunadhihirisha jinsi ambavyo fasihi hususan tendi zinavyofungamana na tamaduni za Kiafrika.

## 1.0 Utangulizi

Utendi ni utanzu wa kifasihi wenye historia ndefu katika fasihi ya Kiswahili na Kiafrika kwa ujumla. Kutokana na historia yake, utanzu huu umechunguzwa na wataalamu mbalimbali na ambao tafiti zao zimezua mijadala anuwai. Mijadala hiyo imeanzia katika jina la utanzu wenyewe na kuendelea katika vipengele mbalimbali kama vile kuwapo kwa utendi Afrika, sifa za utendi, suala la shujaa na matumizi ya sihiri katika tendi (taz. Mulokozi, 1996; Deme, 2009; Faki, 2015; Mtega, 2015; Mahenge, 2016 na Mwagike na Omari, 2016). Katika makala haya hatukumakinikia mambo yote hayo, bali tumeshughulikia kipengele cha sihiri na jinsi kinavyosawiriwa katika tendi.

Kwa mujibu wa Segal (1981), hakuna fasili ya jumla kuhusu dhana ya sihiri inayoweza kutumika mahali pote. Hii ni kwa sababu sihiri haiwezi na haipaswi kutazamwa kama dhana yenye ukweli wa namna moja tu, yaani yenye maana

[1] chrislucas04423@live.com & Kadallahr@yahoo.com

funge. Maelezo ya mtaalamu huyu yanadokeza kuwa maana ya sihiri inabadilika kulingana na muktadha wa matumizi. Kwa msingi huo, hakuna namna moja ya kuifasili sihiri kwani fasili zote zinategemea mtazamo wa tamaduni za jamii husika. Katika makala haya tumetumia fasili ya Janzen na Gaffey (1974) wanaofafanua kuwa sihiri ni nguvu zinazotumiwa na watu wenye maarifa maalumu kwa lengo la kuleta bahati ya mtu, kutibu, kudhuru wengine au kujilinda na maadui kimazingara. Kwa mantiki hiyo, sihiri inarejelea mambo mbalimbali yanayohusishwa na nguvu za asili zipitazo zile za kibinadamu. Maelezo hayo yanaonesha kuwa sihiri ni dhana pana ambayo ndani yake ndimo tunaweza kupata uchawi na uganga.

Jamii nyingi za Kiafrika zimekuwa zikiamini katika sihiri tangu enzi za kale kwa sababu sihiri imekuwa ikihusishwa na masuala muhimu ya jamii kama vile uhai na kifo (Tempels, 1959). Hii inamaanisha kuwa sihiri ni miongoni mwa amali zinazotumiwa na wanajamii kukabiliana na changamoto mbalimbali katika maisha yao. Kwa vile fasihi ni zao la jamii, kazi za kifasihi zimekuwa zikiakisi mambo mbalimbali yaliyomo katika jamii kama vile siasa, imani, mila, dini na falsafa. Aidha, kipengele cha sihiri kimekuwa kinajitokeza sana katika tendi kadha wa kadha za Kiafrika. Katika tendi hizo, sihiri imekuwa ikisawiriwa katika sura mbalimbali. Bila shaka, sura hizo ndizo zilizosababisha baadhi ya wataalamu wa Kimagharibi na wa Kiafrika kutofautiana kimawazo kuhusu uamilifu wa sihiri katika tendi. Wapo wataalamu wanaoona kuwa matumizi ya sihiri katika tendi hayana umuhimu wowote zaidi ya kudumaza tendi kwa kudhoofisha wahusika wake hususan shujaa (Bowra, 1964; Zumthor, 1983). Kwa upande mwingine, wapo wataalamu wanaokweza matumizi ya sihiri katika tendi kwa kuona kuwa sihiri ni kitu muhimu na chenye uamilifu wake katika tendi (Okpewho, 1979; Deme, 2009 na Mulokozi, 2012).

Bowra (1964) na Zumthor (1983) ni miongoni mwa wataalamu wa awali waliotilia shaka matumizi ya sihiri katika tendi. Wataalamu hawa wanadai kuwa tendi za Kiafrika zinaweka msisitizo mkubwa katika matumizi ya sihiri wakati ambapo sihiri inamdhoofisha shujaa na kumfanya aonekane kiumbe dhaifu asiyeweza kufanikisha lolote pasipo na sihiri. Bowra (*khj*) anashadidia kuwa matumizi ya sihiri katika tendi humchora shujaa kama mtu asiyeweza kujitegemea zaidi ya kutumia sihiri. Kutokana na hali hiyo, wataalamu hawa wanawabeza mashujaa wa Kiafrika kwa kuwaona kuwa sio mashujaa halisi kwa sababu ya kutegemea sihiri zaidi kuliko nguvu zao wenyewe.

Mawazo ya Bowra (1964) na Zumthor (1983) yamepingwa na wataalamu mbalimbali wa Kiafrika kama vile Idowu (1973), Deme (2009) na Mulokozi

(2012) ambao wanaona kuwa sihiri ni kipengele muhimu katika tendi za Kiafrika na hakipaswi kupuuzwa. Hii ni kwa sababu sihiri imefungamana na utamaduni wa jamii za Kiafrika. Vivyo hivyo, hata tendi za Kiafrika zimefungamana na utamaduni wa Kiafrika. Kadhalika, wataalamu hawa wanashikilia msimamo kuwa sihiri ni miongoni mwa sifa maridhawa za shujaa ambazo humsaidia katika kukabiliana na vikwazo mbalimbali. Kutokana na hoja hizo wataalamu hawa wanaona kwamba matumizi ya sihiri katika tendi hayapaswi kubezwa kwa namna yoyote ile.

Kutokana na kuwapo kwa mitazamo tofauti kuhusu matumizi ya sihiri katika tendi, makala haya yanaona kuwa msingi wa mgongano uliopo baina ya makundi yanayohusika unatokana na jinsi sihiri inavyosawiriwa. Kadhalika, katika makala haya tunatoa hoja na kupendekeza msimamo kwamba mgongano wa mawazo kuhusu suala la sihiri katika tendi za Kiafrika ulichochewa na kukosekana kwa kiunzi mwafaka cha kinadharia. Ili kulikabili jambo hili, makala yanaangazia usawiri wa sihiri katika utendi mahususi wa Kiafrika kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe.

## 2.0 Misingi ya Nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe

Uchambuzi na uhakiki wa kazi yoyote ya kifasihi lazima uongozwe na misingi madhubuti ya kinadharia. Kama ilivyokwishadokezwa hapo awali, katika makala haya mjadala kuhusu usawiri wa sihiri katika utendi wa *Rukiza* umetekelezwa kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe. Nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe iliasisiwa na kuanza kutumiwa kwa mara ya kwanza na Frans Roh mwaka 1925. Nadharia hii iliibuka baada ya kuona kwamba nadharia tangulizi hususan Nadharia ya Uhalisi ilikuwa imeshindwa kuyaeleza mambo mbalimbali yaliyopo katika jamii, ikiwamo ujitokezaji wa sihiri katika fasihi. Kwa mujibu wa Senkoro (2007), Uhalisia Mazingaombwe ni aina ya fasihi ambamo mazingaombwe au mambo yasiyokuwa ya kawaida kwa hadhira hutokea sambamba na yale ambayo ni ya kawaida. Nadharia hii huchanganya uhalisi na usohalisi katika kuwasilisha mambo mbalimbali yaliyopo katika jamii. Vielevile, nadharia hii inakiuka sifa za uhalisia kama zilivyozoelezwa na waandishi wa Nadharia ya Uhalisia mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni karne ya 20. Nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe husawiri matukio na mambo yasiyoaminika kama yale ya ajabuajabu, fantasia au kichawi kisha kuyaweka sambamba na yale yaliyozoeleka.

Nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe ina misingi mbalimbali lakini katika makala haya, tumetumia msingi mmoja unaosisitiza kuwa vipengele vya kifantasia kama vile sihiri, miujiza na uajabuajabu hutumiwa na wasanii kwa minajili ya kuzua athari mahususi za kiujumi na kijamii. Msingi huu

umetuongoza vyema katika kubaini jinsi sihiri inavyosawiriwa katika tendi kwa kuzingatia mambo mbalimbali ambayo yanahusishwa na nguvu za asili na yasiyo ya kawaida katika muktadha halisi wa utendi uliochunguzwa.

### 3.0 Usawiri wa Sihiri katika Utendi wa *Rukiza*

Sehemu hii imeangazia jinsi sihiri inavyosawiriwa katika utendi wa *Rukiza*. Katika kukamilisha azma hiyo, tumeongozwa na Nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe kama ilivyoelezwa hapo juu. Aidha, makala haya yamebaini kuwa sihiri katika utendi wa *Rukiza* imechukua nafasi kubwa sana na katika kufanya hivyo tumeona kuwa sihiri imesawiriwa katika sura tofautitofauti kama vile miujiza, siri, nguvu za ajabu, sadaka, ndumba na ramli. Matumizi ya sihiri katika utendi huu yameonekana katika muundo mzima wa tendi husika tangu kuzaliwa kwa shujaa mwenyewe hadi kuuawa kwake kama inavyodokezwa katika muhtasari hapa chini:

### 3.1 Muhtasari wa Utendi wa *Rukiza*

Utendi wa *Rukiza* ni miongoni mwa tendi za *Nanga* ambao ulitambwa na Yeli Habibu Selemani mwaka 1974 kwa lugha ya Kihaya na kisha kutafsiriwa na Mulokozi kwa lugha ya Kiswahili (Mulokozi, 2002). Utendi huu unasimulia habari za shujaa Rukiza kuanzia kuzaliwa kwake, harakati za ukombozi wa jamii ya Baganga na kufa kwake. Utendi unaanza kwa kueleza tukio la kuzaliwa kwa shujaa Rukiza ambalo lilitawaliwa na miujiza mbalimbali. Baada ya shujaa kuzaliwa alianza mikakati ya kuikomboa jamii ya Baganga kwa kuwasafirisha na kuwapeleka katika nchi ya baba yao. Katika safari hiyo, shujaa Rukiza alikumbana na vikwazo mbalimbali lakini alitumia sihiri kukabiliana navyo. Kwa mfano, shujaa alitumia mkojo kuwapofusha Vinyambo waliomzuia kupita katika mto. Baada ya shujaa kuwafikisha Baganga katika nchi yao ya asili, aliweza kujenga himaya ya Baganga na kufanikiwa kuondoa ufukara waliokuwa nao. Katika utendi huu, tunaeleza kuwa Rukiza alipigana vita mara mbili na hasimu wake, Ruhinda. Katika pambano la kwanza, Rukiza alishinda kutokana na kuwa na roho tatu ambazo ndiyo sihiri yake. Mwishoni, tunaelezwa kuwa mtoto wa Rukiza alivujisha siri ya sihiri ya baba yake, suala lililosababisha kuangushwa kwa utawala wake.

### 3.2 Njia au Vipashio vya Kisanaa Vilivyotumika Kusawiri Sihiri

Sehemu hii imeangazia jinsi sihiri inavyosawiriwa katika utendi wa *Rukiza*. Katika kukamilisha azma hiyo, tumeongozwa na Nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe kama ilivyoelezwa hapo juu. Aidha, makala haya yamebaini kuwa sihiri katika utendi wa *Rukiza* imesawiriwa katika sura tofautitofauti kupitia mbinu au vipashio mbalimbali vya kisanaa kama vile miujiza, siri, nguvu za ajabu, sadaka, ndumba na ramli. Nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe

imetuwezesha kutambua kuwa ingawa mambo yote yamejitokeza kwa njia ya kiuajabuajabu, yanapotumika katika tendi yametumika kuwasilisha fikra halisi za kijamii ikiwamo kumpambanua shujaa wa kiutendi katika jamii husika kama inavyodhihirika katika sehemu zifuatazo za makala haya.

### 3.2.1 Usawiri wa Sihiri kwa Njia ya Kimiujiza

Muujiza ni jambo ambalo si la kawaida na ni vigumu kulithibitisha kwa kutumia kanuni za kijarabati. Katika utendi wa *Rukiza*, kuna miujiza mbalimbali inayojitokeza kama njia mojawapo ya kusawiri sihiri. Miujiza hiyo imejitokeza wakati wa kuzaliwa kwa shujaa na wakati shujaa anapokabiliana na changamoto mbalimbali. Miongoni mwa miujiza iliyotokea wakati wa kuzaliwa kwa shujaa ni kuongea akiwa tumboni mwa mama yake na kitovu cha shujaa kukatwa kwa shoka. Nukuu ifuatayo inadhihirisha suala hilo:

**20. Tandaza majani ya kukalia sebuleni**
**21. Kisha keti unizae**
**22. Ukinicheleweshа nitakupasukia tumboni!"**
**85. Halafu chukueni ngozi yake iwe ndiyo mbeleko yangu**

Katika nukuu hiyo, tunaelezwa jinsi Rukiza alivyokuwa anamwamrisha mama yake kabla hata ya kuzaliwa. Katika mshororo wa 20 na 21 Rukiza akiwa tumboni anamuamuru mama yake kutandaza majani chini kisha aketi ili aweze kumzaa. Aidha, katika mshororo wa 22, Rukiza anamtisha mama yake kwa kumwambia kwamba asipofanya hivyo atampasukia tumboni. Suala la mtoto kumwamrisha mama yake ni kinyume na falsafa ya Kiafrika ambapo mama ndiye anapaswa kuamuru mtoto wake. Hali hii inadokezwa hata katika Nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe kuwa mambo mengi yanayohusishwa na sihiri huwa yapo kinyume na uhalisia. Sambamba na hilo, muujiza mwingine ulitokea pale shoka lilipotumika kukata kitovu cha shujaa baada ya njia za kawaida kushindwa kama inavyonukuliwa hapa chini:

**95. Wakajaribu vyembe vya mianzi vikateleza**
**96. Wakajaribu kisu cha kunyolea hakikufaa**
**97. Siku hiyo kitovu kilikatwa kwa shoka**
**98. Baganga wakasema, “Huyu si mtoto, ni kioja!”**
**99. Huyu si mtoto ni kioja** (uk. 15)

Katika dondoo hilo, mshororo wa 95 na 96 tunaelezwa kuwa vyembe vya mianzi na kisu vilishindwa kukata kitovu cha shujaa baada ya kuzaliwa. Aidha, mshororo wa 97 umetumika kusisitiza kuwa shoka ndicho kifaa pekee kilichoweza kukata kitovu cha shujaa. Suala hili ni kinyume na uhalisia kabisa kwani katika hali ya kawaida kitovu cha mtoto mchanga hakiwezi kuwa kigumu kiasi cha kushindwa kukatwa na wembe au kisu. Hali hii inaonesha ni

kwa jinsi gani miujiza inavyoweza kuwa njia ya kusawiri sihiri ya shujaa wa kiutendi.

Kutokana na ufafanuzi huo, ni dhahiri kuwa sihiri inayojitokeza kama miujiza si matokeo ya akili za mwanadamu kwani Rukiza alikuwa anatenda miujiza hiyo akiwa hana utambuzi wowote. Ontolojia ya Kibantu inaeleza suala hili vyema kuwa wahenga na mizimu inahusika na kutoa msaada wa nguvu ya kudhuru, kulinda na kutenda miujiza mbalimbali (Mbiti, 1969). Kwa msingi huo, ni dhahiri kuwa sihiri iliyojitokeza kwa njia za kimiujiza inatokana na wahenga na wala si akili ya mhusika anayetenda miujiza hiyo. Ujitokezaji wa miujiza hiyo pia unaashiria kuwa mashujaa wa Kiafrika wametangamana mno na mizimu au wahenga wa jamii zao.

Kwa mujibu wa Sosoo (2017), uzazi wa shujaa huambatana na mambo mengi ambayo ni ya kimiujiza na ambayo si ya kawaida katika ulimwengu halisi. Suala hili limejidhihirisha vyema katika utendi huu kutokana na miujiza mbalimbali iliyotokea wakati wa kuzaliwa kwa shujaa Rukiza kama ilivyokwishaelezwa. Kwa kawaida mtoto huanza kuongea baada ya kuzaliwa na pale anapoanza kupata utambuzi, lakini katika utendi huu shujaa anaanza kuongea akiwa bado yupo tumboni mwa mama yake suala ambalo lipo kinyume na uhalisia. Aidha, muujiza huu hauishii kwa mtoto kuongea akiwa tumboni bali unaenda mbali zaidi pale mtoto anapomwamrisha mama yake kufanya mambo mbalimbali ndipo aweze kuzaliwa.

### 3.2.2 Usawiri wa Sihiri kwa Njia ya Kutoa Sadaka

Kwa mujibu wa BAKITA (2015), sadaka ni mali hasa fedha ambayo hutolewa na mtu kwa Mungu ili kupata thawabu. Vilevile, BAKITA (2015) wanaeleza kuwa sadaka inaweza kuwa chakula hususan nafaka, nyama, pombe au damu ambayo hutolewa kwa mizimu ili kuwashukuru, kuwaomba msaada au kuomba msamaha. Maelezo haya yanatujuza kuwa sadaka hutolewa kwa mtu husika na kwa madhumuni maalumu. Katika utendi huu, Rukiza alitoa sadaka kwa mizimu ili kuibariki kaya yake ya Baganga. Sadaka hii ilitolewa kwa njia ya kumuua mtwana ambaye hakuwa na kosa lolote kama inavyonukuliwa hapa chini:

**167. Akavuta upinde asubuhi na kumwua kwa mshale.**
**168. Watu wakauliza, "Rukiza, Mbona umemwua mtwana?"**
**169. Akajibu, "Hiyo ni sadaka ya kaya yetu**

Katika nukuu hapo juu hususan kupitia mshororo wa 167 na 168 tunaelezwa kuwa Rukiza alimuua mtwana kwa kutumia mshale. Aidha, katika mshororo wa 169 Rukiza anathibitisha kuwa amemuua mtwana kwa ajili ya kutoa sadaka

kwa wahenga ili kaya yake ibarikiwe. Nia hiyo, ndiyo inadhihirisha kuwa suala hili linahusishwa na sihiri. Kwa mujibu wa Bourdillon (1990), utoaji sadaka kwa wahenga ni kitendo kinachohusishwa na sihiri. Sadaka kama njia mojawapo ya kudhihirisha sihiri ya shujaa inaonesha ni kwa jinsi gani Waafrika huwakumbuka wahenga wanapokumbwa na majanga ya namna mbalimbali. Suala hili pia limekuwa likijitokeza hata katika jamii zetu pale kunapokuwa na shida ambazo zipo juu ya uwezo wa binadamu kama vile ukame. Katika mazingira hayo, watu hutoa sadaka ya kuchinja mifugo ili kuweza kupata mvua. Kwa msingi huo, usawiri wa sihiri katika tendi unaendeleza utamaduni wa Kiafrika kama Deme (2010) anavyosisitiza kuwa matumizi ya sihiri kwa shujaa ni kama dira inayoakisi na kuendeleza tamaduni za Kiafrika. Aidha, sadaka kama njia ya kusawiri sihiri katika utendi wa *Rukiza* imetusaidia kutambua jinsi shujaa wa tendi za Kiafrika anavyofungamana na jamii yake, siyo tu jamii ya watu walio hai bali hata jamii pana ya mizimu na wahenga.

### 3.2.3 Usawiri wa Sihiri kwa Njia ya Ramli

Amar (2015) anaeleza kwamba upigaji ramli unarejelea njia ya mawasiliano kati ya wanadamu na nguvu zilizo juu ya uwezo wao ili kupata maarifa fulani ambayo yamefichwa. Amar (2015) anaendelea kudai kuwa upigaji ramli ni tukio la kisihiri ambalo huhusisha vifaa mbalimbali kama vile mkia, mnyama, ungo, mawe ya baharini na manyoya. Katika utendi wa *Rukiza*, upigaji ramli ni njia mojawapo iliyotumika kusawiri sihiri. Aidha, upigaji ramli huo ulihusisha utumbo wa kuku kama kifaa cha kupigia ramli. Suala la kupiga ramli lilikuja baada ya mfalme Ruhinda kugundua kuwa shujaa Rukiza ana uwezo ambao si wa kawaida kama inavyodondolewa hapa chini:

**533. Ruhinda akasema "Niitieni mbashiri wangu"**
**536. Wakakamata kuku Mchakuraji-Mkeshaji**
**537. Wakapiga ramli, utumbo wa kuku ukawa mweusi**
**540. Wakasema "Ewe Mfalme uliyetaka, tulichokiona ni hiki:**
**541. Ewe Mpaji, ukitaka kumwua Rukiza**
**542. Itabidi kwanza upose na kuoa katika nyumba yake (uk.25)**

Katika dondoo hapo juu hususan mshororo wa 533 na 537 tunaonyeshwa jinsi tukio la kupiga ramli lilivyotendeka, muktadha uliosababisha haja ya kufanya ramli, na matokeo ya ramli husika. Kwa ufupi, baada ya Ruhinda kugundua kuwa shujaa Rukiza ana uwezo ambao si wa kawaida, alimwita mbashiri wake ili aweze kupiga ramli kugundua siri ya uwezo huo. Ramli yenyewe ilipigwa kwa kutumia utumbo wa kuku. Aidha, mshororo wa 540-542 unadokeza matokeo ya ramli hiyo kuwa kama mfalme anataka kumuua Rukiza anapaswa

kumposa binti wa Rukiza. Ramli kama njia ya kusawiri sihiri inaonesha jinsi ambavyo wanajamii hutumia sihiri katika kutatua changamoto mbalimbali pamoja na kupata maarifa yaliyofichwa. Hali hii inaonesha kuwa katika sanaa ya tendi si shujaa pekee ambaye anatumia sihiri, bali hata wahusika wengine hutumia sihiri katika kukabiliana na mambo mbalimbali. Kwa msingi huo, madai ya Bowra (1964) yanayoelekea kupinga matumizi ya sihiri kwa mashujaa wa Kiafrika yanapaswa kusailiwa kwa misingi ya kinadharia na kiuchambuzi ili kuona ubora na udhaifu wake. Aidha, katika makala haya tunatoa hoja kuwa madai ya wataalamu mbalimbali wanaopinga matumizi ya sihiri katika tendi yana lengo la kumdhoofisha shujaa wa Kiafrika na kumtenga na tamaduni zake pamoja na wahusika wengi wa kiutendi.

### 3.2.3 Usawiri wa Sihiri kwa Njia ya Siri

Kwa mujibu wa Mahenge (2015) mashujaa huwa na siri fulani inayohusu nguvu za ushujaa wao. Aidha, siri hiyo haipaswi kujulikana kwa adui wa shujaa kwani inaweza kutumika kama silaha ya kumwangamiza. Makala haya yamebaini kuwa siri hiyo ni njia mojawapo ambayo imetumika kusawiri sihiri. Katika utendi wa *Rukiza*, shujaa alikuwa na siri ambayo inahusishwa na uwezo alionao. Suala hili linaelezwa vyema katika nukuu ifuatayo:

> **598. "Kwa nini baba yako anapochomwa mkuki hafi?"**
> **599. Nikaona anamjibu, "Roho yake ipo kwenye kilele cha nyumba**
> **600. Nyingine ipo kwenye mgomba wa *ntundu***
> **601. Nyingine ipo kwenye muoto wa watoto."**

Katika beti zilizonukuliwa hapo juu, tunaelezwa kuwa Rukiza alikuwa ana siri iliyodhibiti ushujaa wake. Siri yake ilihusu roho tatu alizokuwanazo shujaa huyo. Aidha, roho hizo zilimlinda asiweze kudhurika. Mishororo ya 599, 600 na 601 inadhihirisha kuwa roho za Rukiza zilikuwa zimehifadhiwa katika mazingira tofautitofauti kama vile kwenye mgomba wa ntundu, kwenye paa la nyumba na kwenye muoto wa watoto. Hivyo, siri hii inamtaka adui wa shujaa kufahamu kwanza sehemu halisi ambapo roho hizo zimehifadhiwa ndipo amuue shujaa. Aidha, suala la mtu kuwa na roho tatu ni la kiajabuajabu na ambalo lipo kinyume na uhalisia. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe vipengele vya kiajabuajabu vinaweza kutumika kuakisi masuala halisi ya kijamii. Katika utendi huu, kitendo cha shujaa kuwa na roho zilizo nje ya mwili wake kinathibitisha ushujaa wake.

Kadhalika, siri kama njia mojawapo ya kusawiri sihiri inadhihirisha kuwa ushujaa unategemea sana maarifa yaliyofichwa kama tulivyodokeza hapo awali katika fasili ya sihiri. Hali hii ndiyo imewafanya baadhi ya wataalamu kama

Bowra, (1964) na Zumthor (1983) kubeza matumizi ya sihiri, bila kufahamu kuwa sihiri ni maarifa waliyonayo watu wachache tu. Aidha, umuhimu wa sihiri unaweza kudhihirika vyema kwa watumiaji au wanajamii ambao wanaamini kuwa sihiri ni sehemu ya utamaduni wao.

### 3.2.4 Usawiri wa Sihiri kwa Njia ya Nguvu za Ajabu

Ni suala la kawaida watu kuwa na nguvu ambazo zinawasaidia katika kukabiliana na mambo mbalimbali. Aidha, nguvu hizo huenda na umbo, umri na hata jinsia ya mtu husika. Wakati mwingine nguvu hizi huvuka mpaka wa uhalisia na kumwezesha mtu kutenda mambo ambayo si ya kawaida. Ni wakati huu ambapo nguvu hizo hugeuka na kuwa nguvu za ajabu ambazo katika utendi huu zimetumika kama njia ya kusawiri sihiri. Katika utendi wa *Rukiza*, shujaa Rukiza alikuwa na nguvu za ajabu ambazo zilimwezesha kutenda mambo mbalimbali yasiyo ya kawaida na ambayo hayajazoeleka kama inavyojidhihirisha katika nukuu ifuatayo:

**108. Wakampitisha dume huyo pale sebuleni**
**109. Nikaona Mtoto anainua kijikono chake**
**110. Akampiga dume kigumi chake**
**111. Nikaona dume huyo anaanguka mweleka karibu na muoto**
**113. Wakasema, “Nendeni mlete visu”**
**114. Baganga wakaenda kutafuta visu**
**115. Waliporudi walikuta kimekwisha mchinja dume kwa vidole vyake**
**116. Walikuta kimeshachinja na kula nyama!** (uk. 15)

Katika nukuu hiyo, tunaelezwa jinsi Rukiza alivyonyanyua mkono na kutumia kigumi chake kumpiga ng'ombe mpaka akaanguka. Mtunzi ametumia neno kigumi katika mshororo wa 110 ili kudhihirisha kuwa Rukiza alikuwa bado ni mtoto mdogo, hivyo, hata ngumi yake ilikuwa bado ndogo. Pia, tunaelezwa jinsi Rukiza alivyochinja dume la ng’ombe kwa kutumia vidole vyake (mshororo wa 155-116). Mambo yote haya yanaonyesha jinsi sihiri inavyoweza kujitokeza kama nguvu za ajabu alizonazo shujaa kupitia mkono wake. Mkono wa shujaa umetumika kufanya mambo ya ajabu ambayo ni kinyume na uhalisia. Katika hali halisi ng’ombe huchinjwa kwa kutumia zana maalumu kama kisu au panga. Vilevile, ng’ombe dume anaweza kuangushwa kwa kufungwa kamba na kuvutwa na mtu zaidi ya mmoja, lakini katika tukio hili mambo yapo kinyume na uhalisia. Kufuatia hali hiyo, makala haya yanatoa hoja kuwa nguvu za ajabu walizonazo mashujaa huwatofautisha na wahusika wengi.

Nguvu za ajabu alizokuwa nazo Rukiza zilimwezesha kupambana na hasimu wake, Ruhinda. Katika pambano hilo, tunaelezwa kuwa wanajeshi wa Ruhinda walikuwa 6000, lakini kutokana na nguvu za ajabu alizokuwa nazo Rukiza, aliweza kuua wanajeshi 5940 na kubakisha wanajeshi 60 ili waweze kurudisha taarifa kwa Ruhinda. Suala hili linathibitika vyema katika nukuu ifuatayo:

**525. Rukiza ametuua akatumaliza**
**526. Tulikwenda watu magana sitini**
**527. "Ewe mfalme wangu, tumerejelea sitini tu!**
**528. (Magana sitini ndio kusema kila *igana* ni mia moja)**
**529. Eeee ai maskini.** (uk.25**)**

Katika nukuu hiyo, tunaelezwa jinsi Rukiza alivyowaua wanajeshi wengi, suala lililomfanya Ruhinda kubaini kuwa Rukiza hakuwa na nguvu za kawaida. Suala la mashujaa kuwa na nguvu nyingi limesisitizwa na wahakiki wengi wa tendi hususan Johnson (1986), Wamberia (1989), Mulokozi (1999), Wamutiso (1999) na Kazinja (2017). Wataalamu hawa wamebainisha sifa mbalimbali za shujaa ikiwa ni pamoja na nguvu nyingi. Hata hivyo, sihiri inayosawiriwa kama nguvu za ajabu ndiyo huwafanya mashujaa kuwa na nguvu nyingi. Kwa msingi huo, baadhi ya sifa za shujaa wa Kiafrika hupambanuliwa na sihiri. Hivyo, kitendo cha kumtenga shujaa wa Kiafrika na sihiri ni kumfanya apoteze uhalisia wake.

### 3.2.5 Usawiri wa Sihiri kwa Njia ya Ndumba

Kwa mujibu wa TUKI (2013), ndumba ni dawa anayopewa mtu kwa ajili ya kumlinda au kumdhuru. Katika utendi wa *Rukiza*, ndumba imetumika kama njia ya kusawiri sihiri ambapo mtoto wa Rukiza alipewa ndumba za kumpumbaza ili aweze kusema siri ya sihiri ya baba yake. Suala hili lilitokea baada ya Ruhinda kuona kuwa shujaa Rukiza ana nguvu za ajabu. Hivyo, waliamua kupiga ramli na kubaini kuwa Ruhinda alipaswa kuoa mtoto wa Rukiza kisha kumfanyia ndumba ili aweze kusema siri ya baba yake. Suala hili linadhihirika vyema katika nukuu ifuatayo:

**586. Mpe mwali ndumba hizi**
**587. Azitundike kwenye nguzo tatu za *kilela***
**591. Wakasema, "Utakapoona ameitundika**
**592. Na ukipanda katika nyumba ya kulala**
**593. Mwali atakueleza siri za nyumbani kwao."**
**594. Mukama akazileta zile ndumba**

Nukuu hiyo, inaonesha jinsi mtoto wa Rukiza alivyopewa ndumba ili kuweza kutoboa siri ya baba yake. Aidha, ndumba kama njia ya kusawiri sihiri inadokeza kuwa sura mbalimbali za sihiri zinaingiana kwa namna moja au

nyingine. Katika sehemu hii, tunaona kuwa siri, ramli na ndumba zinaingiliana katika utendaji wake. Kadhalika, sihiri kama ndumba inaonesha namna ambavyo shujaa hatakiwi kubweteka na sihiri yake kwani kuna sihiri yenye nguvu zaidi ambayo inaweza kutumika katika kubaini udhaifu wa shujaa. Kwa msingi huo, si kweli kwamba sihiri humfanya shujaa abweteke, bali humfanya shujaa kuwa makini zaidi kwa kujua kuwa hata hasimu wake anaweza kutumia sihiri yenye nguvu zaidi kukabiliana naye.

## 4.0 Hitimisho

Makala haya yametalii jinsi sihiri inavyosawiriwa katika sanaa ya tendi. Nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe ndiyo imetuongoza kubainisha vipashio vya kisanaa au njia mbalimbali zilizotumika kuakisi hali mbalimbali za sihiri. Makala haya yamebaini kuwa sihiri ya shujaa huwa inasawiriwa kwa kutumia njia mbalimbali kama vile ndumba, siri, miujiza, nguvu cha ajabu, ramli na sadaka. Aidha, njia zote hizi zimefungamana na uwasilishwaji wa hali halisi ya kijamii ikiwa ni pamoja na kupambanua nduni bainifu za shujaa. Pia, zimefungamana na utamaduni wa jamii ya Waafrika. Vilevile, tumebaini kuwa si shujaa pekee anayetumia sihiri katika tendi bali hata hasimu wake pamoja na wahusika wengine wanatumia sihiri. Kwa msingi huo, tunapochunguza sihiri katika tendi hatupaswi kumuangalia shujaa pekee, bali tunapaswa kutalii utendi nzima, ikiwa ni pamoja muktadha uliozua utendi husika. Hii itatuwezesha kuchunguza nafasi ya sihiri kwa usahihi zaidi kuliko kumuangalia mhusika mmoja, tena bila kumuunganisha na muktadha wa tendi husika. Kwa ujumla, kutokana na matokeo yaliyopatikana tunahitimisha kuwa sihiri ndiyo sifa ya kipekee ya kisanaa yenye uwezo wa kupambanua nduni anuwai za shujaa wa kiutendi. Watafiti wanapaswa kuendelea kukichunguza kipengele hiki kwa umakini mkubwa. Umakini wa tafiti hizo ujumuishe uteuzi wa nadharia mwafaka na kuzingatia muktadha ambamo kazi ya kisanaa imechimbuka.

## Marejeleo

Amar, A. (2015). *Vocabulary for the Study of Religion.* Boston: Brill.

Bourdillon, M. (1990). *Religion and Society*. Gokomere: Mambo Press.

Bowra, C. M. (1964). *Heroic Poetry*. London: Macmillan.

Deme, M. K. (2009). *The Supernatural in the African Epic Traditions as a Reflection of the Religious Beliefs of African Societies*. Michigan: Western Michigan University Press.

Faki, M. A. (2015). Kuchunguza Sifa za Kifani za Utendi wa Kiswahili. Mfano *Utendi* wa *FumoLiyongo*. Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Idowu, E. B. (1973). *African Traditional Religion: A Definition Maryknoll*. Nigeria: N. Y. Orbis Books.

Janzen, J. M. na Gaffey, W. (1974). “An Anthology of Kongo Religion”. *Athropology*, Juz. Na. 5: 163-194.

Johnson, J. W. (1986). *The Epic of Son-Jara*. Bloomington: Indiana University Press.

Kazinja, G. (2017). Shujaa Mwanamke na Mwanamume Katika Utendi: Uchambuzi wa Utenzi wa *Rasil’ ghuli* na Utendi Simulizi wa *Kachwenyanja.* Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mahenge, O. (2016). Shujaa wa Kiutendi wa Jamii ya Wakinga. Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mtega, W. (2015). Uhusiano wa Taashira na Maisha ya Shujaa wa Kiutendi: Uchunguzi wa Utendi wa *Rasi ‘lGhuli* na Utendi wa *Nyakiruu Kibi*. Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Saalam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (2002). *The African Epic Controversy: Historical, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Epic Poetry and Performance*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Mwagike, A. na Omari, S. (2016). “Tenzi Tafsiriwa katika Kiswahili: Ruwaza ya Shujaa Inavyojenga Falsafa katika Utenzi wa Kalevala”. Katika *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi.* Dar es Salaam: Daud Publishing. Kur. 256-278.

Okpewho, I. (1979). *The Epic in Africa: Towards a Poetics of the Oral Performance*. London: Longman.

Saffari, A. J. (1993). “Uchawi katika Riwaya ya Kiswahili”. Katika *Makala ya Semina ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania.* Dar es Salaam. TUKI. Kur. 260-270.

Segal, A. F. (1981). “Hellenistic Magic: Some Questions of Definitions.” *Studies of Gnosticism and Hellenistic Religions*. Leiden: Brill Press.

Senkoro, F. E. M. K. (2007). “Uhalisia Mazingaombwe katika Fasihi ya Kiswahili: Istilahi Mpya, Mtindo Mkongwe”. Katika *Kioo cha Lugha*.

Shimweta, G. (2015). Itikadi katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa *Ngoma ya Ng’wanamalundi* na *FumoLiongo.* Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Sosoo, F. K. (2017). Ushujaa katika Motifu ya Safari ya Msako: Ulinganishi wa Ngano za Kiewe kutoka Ghana na Riwaya za Shaaban Robert kutoka Tanzania. Tasnifu ya Uzamivu, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Tempels, P. (1945). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.

TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 3). Nairobi: Oxford Universty Press.

Wa Mberia, K. (1989). "Fumo Liyongo". Katika *Mulika*. Juz. Na. 21: 25-43.

Wa Mutiso, K. (1999). "Sira ya Majagina: Buddha na Muhammadi." (Haijachapishwa) Iliwasilishwa katika kongamano la *Swahili Kolloquim Universitat,* Bayreuth. 14/05/1999.

Wa Mutiso, K. (2012). "Motifu ya Hirizi katika Ushairi wa Kiislamu wa Kiswahili". Katika *Mulika*. Juz. Na. 31: 115-135.

Zumthor, P. (1983). *Introduction to Oral poetry*. Paris: Seuil.